

**Barua ya Miadi kwa Idara ya Msaada wa Watoto (DCS)
Uamuzi wa Sababu ya Msingi**
Appointment Letter for Division of Child Support (DCS) Good Cause Determination

Tarehe:

Nambari ya Mteja:

Kwa:

Mpendwa ,

Umeomba Sababu ya Msingi na kuiambia Ofisi yako ya Huduma za Jamii ya karibu nawe kwamba huwezi kuisaidia Idara ya Msaada wa Watoto (DCS) kukusanya matunzo ya mtoto na/au matibabu. DCS hutoa huduma kamili za utekelezaji wa usaidizi ikiwa unapopokea TANF. Huduma hizi zinaweza kujumuisha DCS kuanzisha ubaba, kuingia na/au kutekeleza agizo la msaada, kutekeleza wajibu wa mzazi mwingine ili kutoa bima ya afya na kuchangia sehemu yake ya gharama za matibabu ambazo hazipo kwenye bima kwa watoto wako. Nimetenga miadi ifuatayo ili kuzungumza na wewe kuhusu ombi lako la Sababu ya Msingi ya kusitisha hatua zozote za matunzo ya mtoto na matibabu.

Nimetenga miadi ifuatayo ili kuzungumza na wewe kuhusu ombi lako la Sababu ya Msingi ya kusitisha hatua zozote za matunzo ya mtoto na matibabu.

ANWANI

TAREHE

MUDA

Ikiwa huwezi kuja, tafadhali nipigie kwa _____ kabla ya _____. **Ikiwa hutapiga simu au kuja kwenye miadi yako, naweza kukataa ombi lako la Sababu ya Msingi.**

Nitaidhinisha ombi hili la Sababu ya Msingi ikiwa litaamuliwa:

- Unahofia wewe au watoto unaowatunza watadhurika sana kimwili au kihisia.
- Mtoto wako alizaliwa kwa sababu ya kubakwa au kujamiiiana kwa maharimu.
- Umeanza taratibu za kuasili mtoto, au upo kwenye ushauri (hadi miezi mitatu) na wakala wa uwekaji watoto kuhusu kuasili.

Katika miadi, unaweza kuandika taarifa iliyosainiwa ambayo inaelezea wasiwasi wako na hofu. Unaweza pia kuleta taarifa zingine ili kusaidia ombi lako, ikiwa zinapatikana. Baadhi ya mifano ni kama:

- Ripoti za polisi;
- Ripoti za matibabu;
- Ripoti za mahakama;
- Agizo la ulinzi wa unyanyasaji wa majumbani;
- Taarifa iliyoandikwa kutoka kwa mapadri, marafiki, ndugu, majirani, wafanyakazi wenzio ikieleza hatari hiyo;
- Barua kutoka kwenye makazi ya unyanyasaji wa nyumbani; au
- Barua kutoka kwa washauri wa unyanyasaji wa nyumbani.

Nini hufanyika katika miadi hii?

- Utaweza kueleza kwa nini unahofia kukusanya matunzo ya mtoto na matibabu kunaweza kukudhuru wewe au mtoto wako.
- Tunaweza kuzungumzia usaidizi mwingine unaoweza kuhitaji ili kuwa salama.

Nini kitatokea ikiwa hutatoa taarifa iliyotiwa saina au maelezo mengine kuonyesha kwa nini kukusanya matunzo ya mtoto na matibabu kunaweza kukudhuru wewe au mtoto wako?

- Ombi lako linaweza kukataliwa ikiwa hatutaona kuwa sababu zilizotolewa zinakidhi mahitaji ya kukubali Sababu ya Msingi na
- Kesi yako itatumwa kwa DCS ili kufungua kesi ya matunzo ya mtoto kwa huduma kamili za utekelezaji wa msaada.
- Kunaweza kuwa na wakili wa unyanyasaji wa majumbani katika CSO ya eneo lako au katika jumuiya yako ambaye anaweza kupatikana kuhudhuria mkutano huu pamoja nawe. Wasiliana na CSO ya eneo lako kwa maelezo zaidi.

Je, itakuaje ikiwa hukubaliani na uamuzi wetu?

1. Unaweza kupiga simu kwa Ofisi yako ya Huduma kwa Jamii au kuandika barua kwa Office of Administrative Hearings, PO Box 42489, Olympia WA 98504-2489 ndani ya siku 90 ili kuomba kusikilizwa shauri. Ikiwa utaomba kusikilizwa shauri, DCS haitaanza kushughulikia kesi yako hadi uamuzi wa kusikilizwa shauri uwe wa mwisho. Wakili au mtu mwingine anaweza kukuwakilisha kwenye shauri hilo, au unaweza kujiwakilisha mwenyewe.
2. Ondoa ombi lako la TANF. Hata hivyo, DCS inaweza kushughulikia kesi yako kwa muda uliopokea TANF.
3. Endelea kupokea msaada na usishiriki katika shughuli za utekelezaji wa usaidizi. Hata hivyo, ikiwa hutashiriki katika shughuli za utekelezaji wa msaada DCS itaendelea kushughulikia kesi yako na msaada wako wa pesa unaweza kupunguzwa kwa asilimia 25% ikiwa ombi lako la Sababu ya Msingi litakataliwa.

Wakili au mtu mwingine unaemchagua anaweza kukuwakilisha kwenye shauri hilo, au unaweza kujiwakilisha mwenyewe.

Je, unaweza kupata ushauri wa kisheria au kuwasilisha?

Unaweza kupiga simu kwa laini ya huduma za kisheria ya jimbo zima kwa nambari 1-888-201-1014.